22140197

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI A: LITERATURE – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI A : LITTÉRATURE – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI A: LITERATURA – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Friday 9 May 2014 (morning)
Vendredi 9 mai 2014 (matin)
Viernes 9 de mayo de 2014 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a literary commentary on one passage only.
- The maximum mark for this examination paper is *[20 marks]*.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N’ouvrez pas cette épreuve avant d’y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire littéraire sur un seul des passages.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d’examen est *[20 points]*.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario literario sobre un solo pasaje.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es *[20 puntos]*.


© International Baccalaureate Organization 2014

*Andika uchambuzi kuhusu kifungu **kimoja** kati ya hizi:*

**1.**

Baada ya kazi za kutwa kata, kusanya, buruta, pakia, na kutembea juu chini, alikuwa amechoka tiki. Juma aliwasili nyumbani na moja kwa moja akajitupa kitandani kama gunia baada ya kujimwagia maji ya moto. Usiku huo hakula. Chakula kwake hakikuwa muhimu. Ulichohitaji mwili wake ni pumziko. Usingizi ulimwiba pindi tu kichwa chake kilipodara mto. Alilala kama gogo.

Usiku wa manane, nje kulikuwa kumetanda giza totoro. Wingu zito jeusi liligubika mbingu gubigubi na katu nyota hazikuthubutu kumetemeta kama kawaida. Rasharasha za mvua zilianza kutematema mate ardhini zikiandamana na kibaridi kikali cha kuvunja mifupa.

Bi. Mayeye, mkewe Juma, ndio mwanzo anajivutia blanketi na kupinduka upande wa pili wa kitanda akiogelea katika lindi la usingizi mnono wa pono. Juma naye alizidi kulimatia kitandani huku kanjikunyata mithili ya mwana paka. Huko nje mvua ilivalia njuga, ikachacha si haba ikiandamana na mingurumo na radi kali iliyopenya nyufa za kuta za nyumba ya bwana Juma na kuwapiga waliolala picha za bure. Maji ya mvua sasa yalikuwa yakitiririka katika sehemu fulani za paa la nyumba hiyo ambako makuti yalikuwa yameoza.

Alfajiri mvua ilipusa. Majogoo yalisikika yakipigapiga mbawa – ishara ya kuipokea siku mpya. Juma alibumburuka kutoka usingizini kama aliyebaua kitandani akamsukasuka mkewe ambaye usingizi ulikuwa umemteka akamwita, “Eeeeh bibie, amka nitachelewa na kibarua na mahamri yako leo yatapasuka tuguuni.” Kutajiwa mahamri yake alichomoka mbio kitandani akielekea uani kulikokuwa na jiko lake.

Jikoni kulikuwa kumelowa chepechepe. Alianza kibarua cha kuzoa tope hadi kukawa afadhali. Aliwasha jiko akamtelekea mumewe maji ya kuoga kisha akarudi ndani kumwita na kuwaamsha wanawe wasichelewe kwenda shule. Ahali zake walipokuwa wakijitayarisha alirudi jikoni akaanza kuchoma mahamri yake baada ya kutujia nyungu yake ya mbaazi ambazo huziuza kila siku asubuhi pamoja na mahamri. Hiki pia kilikuwa ndicho kiamshakinywa cha familia yake. Mahamri na mbaazi haikuwa biashara pekee kwa Bi. Mayeye. Alikuwa akipika mabuyu na bisisi ambazo wanawe hupeleka shuleni na jioni yeye mwenyewe hukalia chungu cha uji wa ngano na karai la viazi barazani pake hadi magharibi. Jua likishatua ndipo yeye huingia ndani akahesabu hela alizopata, akapanga za kununua bidhaa zake za biashara kama unga wa ngano, hamari, iliki, sukari, mbaazi, nazi, vitunguu maji nau, dawa ya mchuzi (bizari), ngano nzima, viazi, mafuta ya uto, chumvi na kuni. Pesa zinazosalia hutumia kununua kitoweo, unga wa sima na mafuta ya taa kwa ajili ya familia yake kwani kazi ya mumewe haikuwa na mshahara wa haja. Kwa kuwa ilikuwa kazi ya kijungu jiko ilimbidi Bi. Mayeye ajifunge kibwebwe kimkaze kiunoni amsaidie mumewe kusukuma gurudumu la maisha. Alifahamu maana ya haba na haba hujaza kibaba.

Baada ya kiamshakinywa Juma alitoka shoti kuelekea mjini alikofanya kazi ya ushamba boi katika kampuni moja kubwa. Miale ya jua la asubuhi mbichi kamwe haikuweza kupenya mikono yake katika wingu zito jeusi lililogubika mbingu. Njiani alichapuka chapuchapu huku akirukaruka kama chura kukwepa vidimbwi vya maji ya mvua. Baridi shadidi ilimfanya kutetema kama kifaranga asiye na manyoya. Hakuwa na nguo muhimu ya kujisetiri na baridi. Alivalia kishati kilichochunjuka rangi kwa wingi wa miaka. Kishati chake kwani kilikuwa “chafuka nikufue, kauka ni kuvae”; sio kwa chaguo bali kwa ukata. Suruali yake nayo ilikuwa imekunjana kama iliyotolewa kinywani mwa ng’ombe baada ya kutafunwa. Haijaonana na pasi tangu itoke mitumbani.

Juma aliwasili kazini saa mbili kasorobo akiwa mwingi wa bashasha. Hakujua chanzo cha furaha yote hii. Alijihisi mwepesi na mwenye ali tele ya kuchapa kazi bila gozigozi. Aliwasalimu wafanyi kazi wenzawe wote aliokutana nao huku katandaza tabasamu gego hadi gego. Lakini leo wengi aliokutana nao walionyesha nyuso za wasiwasi. Hilo hata hivyo halikumtia kibuhuti. Alipiga mluzi akielekea stoo kubadili magwada na kuchukua zana zake za kazi, ikiwemo surupwenye aliyoizoea, ikamzoea.

Timothy M Arege, *Gitaa Na Hadithi Zingine* (2011)

**2.**

**Mwana Kazawa**

Mwana ku kwetu lizawa, wakunga lizalishile
Kwa sabuni kaogeshwa, vizuri wamvishile
Kwa sura walivutiwa, jina zuri wampile
Kenya mwanetu kazawa, nane nne nne jina.

Mwana kaliamwa ziwa, vyakula bora alile
Sote humu furahia, kupokea atujile
Wa wote mwenetu kuwa, shimeni tumuenzile
Kenya mwanetu kazawa, nane nne nne jina.

Mwana hatuwa chukuwa, hadi akoomalile
Kitaka kukaa huwa, tanza sota hapa pale
Tainuka kihofiwa, mara chini angukile
Kenya mwanetu kazawa, nane nne nne jina.

Mwana guu tainua, na jingine ajongele
Hivyo kutembeya huwa, kusuwasuwa endele
Kichwa imara takuwa, tachapuka kwenda mbele
Kenya mwanetu kazawa, nane nne nne jina.

Mwanatu ja yai huwa, ndivyo twambile wavyele
Na maradhi kukingiwa, katu zisimwue ndwele
Wa nguvu mlo kupewa, afyaye ahifadhile
Kenya mwanetu kazawa, nane nne nne jina.

Mwana hata kazaliwa, na mguu akosele
Mbali hawi tupiliwa, "chungu mzazi patile"
Mguu mwana tapewa, wa bandia aendelee
Kenya mwenetu kazawa, nane nne nne jina.

Mwana vyo si kukemewa, kwamba huwa hafaile
Kuteleza sio kuwa, kwamba ndiko angukile
Mwanetu kihimiziwa, hatimaye tashindile
Kenya mwanetu kazawa, nane nne nne jina.

Mwana huyu kindaliwa, kwa hii hali na ile
budi kusitawi huwa, kisha kuelekea mbele
Soteni tafurahia, kwayo maanufaile
Kenya mwanetu kazawa, nane nne nne jina.

Mwanetu huyu tatoa, maarifa yafaile
Kwa yeye asochagua, ujuzi aupatile
Si lazima ajiriwa, jua lo kali tanzile
Kenya mwanetu kazawa, nane nne nne jina.

Tama ndimi waye sawa, hapano ndo nikomile
Shime tundumishe kuwa, imara ipendezile
Si wa mbali kutupiwa, na kulaumu vivile
Kenya mwanetu kazawa, nane nne nne jina.

S Kavuna, *Nuru Ya Ushairi Mwongozo Na Uchambuzi* (2009)